ADOLPH KOLPING ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL (AKEMPS)

(Shule ya Msingi Adolph Kolping),
JIMBO KATOLIKI LA BUKOBA,
S.L.P 1236,
Bukoba.

Mawasiliano:
0753 – 822070/0753-190119

Kumb Na. AKEMPS/…….....

Mzazi/Mlezi wa……

YAH: **UTARATIBU WA KUJIUNGA KWA MWANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI MWAKA 2014.**
(DARASA LA KWANZA-SABA)

1. Jumuiya ya Kolping Tanzania inayo furaha kukujulisha kuwa mwanao …….....amechaguliwa/amekubaliwa kuingia darasa la……..katika shule hii mnamo tarehe …… kama mwanafunzi wa kutwa/bweni. Nakupongeza kwa hili.
2. Shule ya Msingi Adolph Kolping iko chini ya Jumuiya ya Kolping Tanzania na lengo lake ni kudumisha maadili mema kwa misingi ya dini, kutoa taaluma kwa viwango vya juu, kujenga moyo wa upendo na umoja kwa wanafunzi wetu ili kujenga Taifa endelevu.
3. Kwa sasa shule hii inapokea wanafunzi wa kutwa na kulala (bweni) lakini baadaye itapokea wanafunzi wa bweni tu, wavulana kwa wasichana, chini ya uangalizi madhubuti unaohakiki nidhamu, amani na usalama wa wanafunzi wa jinsia zote.
4. Shule iko kwenye tambarare za miinuko jirani na Shule ya Msingi Ihungo, nje kidogo ya barabara kuu itokayo Bukoba mjini kuelekea Kashozi, kwa kufuata barabara ndogo inayoelekea shule ya Sekondari Ihungo. Shule yetu iko umbali wa kilometa nane (8) kutoka kitovu cha Manispaa ya Bukoba.
5. **WANAFUNZI WA BWENI (BOARDERS)**

   A. Mwanao atapokelewa na kusajiliwa kuanzia tarehe **13.01.2014** Baada ya kusajiliwa atapewa namba yake ya bweni na kukabidhiwa kwa Matroni/Patroni, ambao watamuonesha mahali pa kulala na kumueleza maadili na sheria za bweni kwa ujumla. Kwa hali hii tutapenda kujua matatizo yote ya pekee yanayomhusu mwanao.

   B. Ada ya masomo, chakula na malazi kwa mwaka, Januari – Disemba ni Tshs. **1,250,000/=,** na zitalipwa kwa awamu tatu au kwa mkupuo kila mwanzoni mwa muhula kama inavyooneshwa hapa chini.
      i. Januari – **420,000/=**
      ii. Mei – **420,000/=**
      iii. Septemba **– 410,000/=**

Malipo yote yalipwe **Benki ya CRDB**, **tawi la Bukoba, Kolping Society of Tanzania,** Namba ya Akaunti, **01J1055942401** na "Bank pay in slip" ikionesha jina la mwanafunzi aliyelipiwa iletwe shuleni kwa uthibitisho. ***Shule haipokei pesa taslimu.***

C. Wanafunzi wanaokuja kuanza watalipa **192,000/=** kwa ajili ya kununua vifaa vifuatavyo:

i.	Shuka 4	24,000/=
ii.	Mto na foronya	6,000/=
iii.	Blanketi 1	15,000/=
iv.	Chandarua 1	6,000/=
v.	Godoro	45,000/=
vi.	Mpira wa mkojo	5,000/=
vii.	Nguo za kushindia	16,000/=
viii.	Nguo za michezo	15,000/=
ix.	Sare (shati 2, kaptula/sketi 2 na sweta 2)	60,000/=
		192,000/=

Tanbihi: Kiasi hicho cha shilingi **192,000/=** (Laki moja elfu tisini na mbili tu) pia kilipwe katika akaunti iliyotajwa hapo juu na "Bank pay in slip" yenye jina la mwanafunzi iletwe shuleni.

D. Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo mbali na vile vilivyotajwa hapo juu:
   i. Taulo 1.
   ii. Ndala jozi 1.
   iii. Nguo za kulalia (Night dress) na jaketi kwa ajili ya baridi.
   iv. Viatu vyeusi jozi 2 visivyo wazi na visivyo na visigino virefu na soksi nyeupe jozi 4.
   v. Chupi 8
   vi. Dawa ya viatu kubwa 1 na brashi 1 (kila muhula)
   vii. Dawa ya meno kubwa 1 na miswaki 2 (kila muhula)
   viii. Ndoo ya lita 10.
   ix. Mafuta ya kujipaka kopo kubwa 1 (kila muhula)
   x. Sanduku au begi la kutosha.
   xi. Kitana kwa ajili ya nywele fupi.
   xii. Vitambaa 2 vyeupe vya mkononi au zaidi.
   xiii. Viatu na soksi za michezo.

E. Tunashauri kila mwanafunzi aje na bima ya afya. Ikishindikana kiasi cha shilingi **25,000/=** kilipwe shuleni kwa ajili ya usajili wa bima ya afya au matibabu kwa mwaka.

F. ***WAGENI:*** Wazazi na ndugu wengine wanaotambuliwa na shule wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi Jumamosi ya kwanza kila baada ya miezi miwili. Ndugu watakaopendekezwa na mzazi/mlezi wasiozidi watano, wataorodheshwa kwenye fomu maalumu ya maombi. Muda wa kutembelea wanafunzi ni kati ya 3:00 asubuhi hadi saa 9:00 mchana.

G. Kama kuna jambo la dharura linalomhusu mwanafunzi unaombwa uwasiliane na uongozi wa shule. Tutashukuru kupata ushirikiano wako wa karibu.

H. Wakati wa kufunga na kufungua shule, ndugu waliodhibitishwa tu wataruhusiwa kumchukua au kumrudisha mwanafunzi shuleni.

6. WANAFUNZI WA KUTWA (DAY SCHOLARS)

A. Mwanao atapokelewa kuanzia tarehe **13.01.2014** na kusajiliwa tarehe hiyo na ataanza masomo mara baada ya mzazi/mlezi kukubaliana na utaratibu wa shule.

B. Kila siku asubuhi mwanafunzi anapokuja shuleni itabidi awe kwenye kituo cha basi kilichopo karibu na nyumbani kwao kwa muda uliopangwa tayari kwa kupanda gari kuja shuleni na alasiri kuanzia 10:30 jioni basi la shule litamrudisha hapo hapo kituoni.

C. Ada kwa ajili ya masomo, chakula na usafiri itakuwa TShs. **980,000/=** kwa mwaka na italipwa kwa awamu tatu au kwa mkupuo kama ifuatavyo:
   i. Januari – **330,000/=**
   ii. Mei – **330,000/=**
   iii. Septemba – **320,000/=**

D. Wasiohusika na usafiri watalipa TShs. **860,000/=** kwa mwaka katika awamu tatu. Ada inaweza kulipwa yote kwa mkupuo kutegemea utashi wa mzazi/mlezi wa mwanafunzi. **Hakikisha unalipa ada husika mwanzoni mwa kila muhula.**
   i. Januari – **290,000/=**
   ii. Mei – **290,000/=**
   iii. Septemba – **280,000/=**

E. Utalipa shilingi **75,000/=** kwa ajili ya sare ya shule ambayo ni: ***shati/blauzi 2 kaptula/sketi 2, sweta 2 na nguo za michezo.***

F. Malipo yote yalipwe **Benki ya CRDB**, **Tawi la Bukoba, Kolping Society of Tanzania,** Namba ya Akaunti, **01J1055942401** na "Bank pay in slip" ikionesha jina la mwanafunzi aliyelipiwa iletwe shuleni kwa uthibitisho. ***Shule haipokei pesa taslimu.***

7. VIFAA MUHIMU (Kwa wanafunzi wa bweni na kutwa)

A. Umnunulie mwanao mfuko wa kubebea vifaa atakavyokabidhiwa ili aje navyo kila siku kwa matumizi ya darasani vikiwa safi.
B. Kila mwanafunzi aje na bunda la karatasi nyeupe (**Ream A4)** ambazo hazina mistari.
C. Utamlipia mwanao shilingi **5,000/=** kwa ajili ya kitambulisho cha shule.
D. Ukarabati – Shilingi **50,000/=**
E. Vifaa vya bwaloni, masomo ya ziada na ziara za masomo – Shilingi **36,000/=**
F. Pesa ya Tahadhali (Caution Money) – Shilingi **20,000/=**

G. Wanafunzi watalipia vifaa vya darasani kama ifuatavyo:
   i. Darasa la kwanza na la pili: **TShs**. **30,000/=**
   ii. Darasa la tatu hadi la saba: **TShs. 40,000/=**

8. <u>MAELEZO MENGINE KWA MZAZI/MLEZI</u>

i. Kuangalia usafi wa mwanao tokea nyumbani kama unaridhisha na kumuandaa aje shuleni akiwa msafi.
ii. Kufuatilia mahudhurio na maendeleo ya mwanafunzi.
iii. Kushirikiana na walimu kurekebisha nidhamu ya mwanafunzi.
iv. Kujitahidi kuhudhuria miito/vikao vya shule bila kukosa.
v. Shule itakuwa na mihula mitatu.
vi. Kama mwanafunzi anafadhiliwa na shirika au mfadhili yoyote mahitaji yake yaombwe mapema kabla mwanafunzi hajawasili shuleni.

9. <u>MAELEZO KWA MWANAFUNZI</u>

i. Kuwahi katika kituo cha basi alichopangiwa na kuhudhuria masomo kila siku.
ii. Kuwa msafi wakati wote kwa mwili na mavazi.
iii. Wizi, tabia za kihuni, ugomvi, pombe, uvutaji sigara, lugha chafu, utumiaji wa madawa ya kulevya n.k havitavumiliwa kabisa.
iv. Mwanafunzi atajifunza masomo yote ya shule za msingi katika lugha ya kiingereza isipokuwa masomo ya Kiswahili na Dini.
v. Mwanafunzi anapaswa kuzungumza lugha ya kiingereza wakati wote akiwa shuleni na anashauriwa kuendeleza tabia hiyo hata akiwa nyumbani mazingira yakiruhusu.
vi. Mwanafunzi asiyehusika na usafiri wa basi awahi shuleni mapema kabla ya saa mbili asubuhi kila siku.
vii. Kila mwanafunzi anatakiwa awatii viongozi wake daima.
viii. Kama itatokea dharura inayomzuia mwanafunzi asije shuleni mzazi atoe taarifa.
ix. Mwanafunzi atafanya mitihani ya kila mwezi na mwishoni mwa kila muhula mzazi/mlezi atatumiwa matokeo yake. (Kwa wanafunzi wote – kutwa na bweni).

10. Wakati mwanafunzi akirudi shuleni awasilishe fumu ya ripoti ikiwa imesainiwa na mzazi/mlezi kila atakapo likizo.

11. Uongozi wa Shule ya Msingi ya Adolph Kolping (AKEMPS)unayo furaha kumkaribisha mtoto wako na kumtakia afya njema na mafanikio katika masomo na malezi kwenye shule hii. Shule itajitahidi kutoa malezi na elimu katika viwango vinavyostahili.

MWALIMU MKUU

JUMUIYA YA KOLPING TANZANIA

JIMBO KATOLIKI LA BUKOBA

SHULE YA MSINGI ADOLPH KOLPING (AKEMPS)

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu na. 25 ya mwaka 1978**, aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini na Jimbo Katoliki la Bukoba. Unatakiwa kuzingatia Kanuni na Sheria hizi kwa kipindi chote utakachokuwa hapa. ***(Maelezo mengine utapewa mara ufikapo shuleni).***

1. Kila mwanafunzi ni lazima kuvaa nguo rasmi za shule *(School Uniform)* wakati wote awapo shuleni na mahali pengine atakapotakiwa kufanya hivyo, hata anapotoka nje ya mazingira ya shule.
2. Ni muhimu na ni wajibu kwa kila mwanafunzi kuwahi bila kuchelewa mahali popote atakapohitajika darasani, kazini, mstarini, n.k.
3. Sala kwa wanafunzi/Jumuiya yote ni lazima shuleni na zitafanyika kwa nyakati zilizopangwa na taratibu zilizowekwa.
4. Juhudi katika kazi za mikono, madarasani na katika michezo ni wajibu wa kila mwanafunzi. Uzembe katika shughuli hizi hautavumiliwa kabisa.
5. Ni wajibu wa mzazi kutoa taarifa endapo mwanafunzi atakosa kuwapo shuleni.
6. Kila mwanafunzi ana wajibu wa kuwaheshimu walimu na walezi, yeye binafsi na kuwaheshimu watu wengine kama anavyopenda kuheshimiwa.
7. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza au kulinda siha na usafi wake binafsi na wa mazingira yote ya shule nje na ndani ya madarasa, vyoo, n.k.
8. Ugomvi au kupigana, kuleta fujo darasani, lugha za matusi, kashfa kwa wenzako au wananchi ni mwiko kabisa.
9. Vipindi vyote vilivyoko kwenye ratiba ni lazima uvihudhurie bila kukosa pamoja na shughuli za nje ya darasa.
10. Kila mwanafunzi sharti aepuke na kuchukia vitendo vyovyote vya uongo, uzushi, wizi, uchoyo, matumizi ya madawa ya kulevya, n.k
11. Lugha inayotumika hapa shuleni ni Kiingereza tu, isipokuwa katika somo la Kiswahili.
12. Mwanafunzi hawapaswi kubisha au kukataa adhabu endapo atavunja sheria za shule.
13. Kila mwanafunzi ni lazima afikishe wastani wa masomo ambao umepangwa ili aweze kupanda darasa.
14. Makoti, vibandiko, vizibau, kofia, kanda mbili, viatu vya wazi, mikanda mipana haviruhusiwi kamwe kuvaliwa wakati mwanafunzi awapo ndani ya vazi la shule.
15. Upole na utii kwa viongozi na walezi ni wajibu kwa kila mwanafunzi; ubishi wenye lengo la kukwepa kutimiza wajibu ni marufuku kabisa.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kupokea au kuhudumia wageni bila ruhusa toka kwa uongozi wa shule.
17. Ni marufuku kuleta chakula shuleni au kupeleka chakula mabwenini.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kuja au kutumia vifaa vya umeme shuleni. Endapo mwanafunzi atakamatwa navyo, adhabu kali itatolewa.
19. Ni marufuku kuchezea na kuharibu mali yoyote ile ya shule.

Tanbihi: Endapo mwanafunzi atavunja sheria na kanuni za shule, adhabu kali itatolewa.

UONGOZI WA SHULE